# Ushairi wa Kiswahili kama Chombo cha Ujenzi wa Utangamano wa KitaifaNchini Kenya

*Joseph Maitaria*
na
*Clara Momanyi*

***Ikisiri***

*Makala haya yanafafanua dhima ya ushairi wa Kiswahili katika kujenga uwiano na utangamano katika jamii. Maendeleo na ustawi wa lugha huenda sambamba na fasihi yake. Ushairi wa Kiswahili kama utanzu wa fasihi, una historia ndefu. Aidha, umaarufu wa ushairi huu hautokani tu na vipengele vya lugha teule zinavyotumika, bali pia ujumbe muhimu unaowasilishwa. Hivyo basi, unaweza kutumiwa kama njia mojawapo ya kujenga utangamano miongoni mwetu. Kasi ya mabadiliko inayosababishwa na mchakato wa utandawazi imeufanya umma wa ulimwengu wa sasa kuangazia athari zake. Ongezeko la uhasama miongoni mwa jamii zetu, vita vya kikabila, tuhuma na ufisadi unaopaliliwa na ubinafsi, ni baadhi ya madhila yanayozikabili jamii za leo hususan katika eneo la Afrika Mashariki. Utangamano mzuri na maridhiano miongoni mwa jamii ni mambo ambayo hayana budi kuzingatiwa ili kuzikomoa jamii zetu kutokana na maovu haya. Katika mazingira haya basi, fasihi inakuwa chombo muhimu cha kujenga utangamano wa kijamii. Ushairi unaweza kutumiwa kama kioo cha kujitazama na kujisaili ili kujijengea ngome ya uwiano na utangamano katika jamii. Kwa mujibu wa muktadha huu basi, swala la utangamano wa kitaifa nchini Kenya linashughulikiwa kwa kurejelea utanzu wa ushairi. Baadhi ya mifano ya mashairi yanayoangazia swala hili inadondolewa ili kulipa uzito unaostahili. Waaidha, makala yanaangazia baadhi ya vipengele muhimu vya kijamii ambavyo vinaweza kushughulikiwa kwa njia hii kwa lengo la kujenga ujamii na utangamano wa taifa.*

---

## 1.0 Utangulizi

Kiswahili ni lugha-zawa ya Afrika Mashariki ambayo imejitanua sio tu kiisimu bali pia kifasihi. Nchini Kenya, uamuzi wa awali wa kukifanya Kiswahili lugha ya taifa ulikusudiwa kuleta maendeleo ya nchi kwa jumla. Aidha, uamuzi wa kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kwanza rasmi nchini kulingana na Katiba ya nchi (2010) ni hatua ambayo itatoa nafasi kubwa zaidi kwa asasi hii kuweza kuendelea na kutekeleza jukumu aali la kuleta uwiano na utangamano wa kitaifa. Tunaporejelea fasihi hususan ya Kiswahili, ni bayana kuwa amba imechangia kwa kiasi kikubwa kuelekeza, kufunza, kuasa na kusisimua jamii. Wanasiasa wametumia fasihi pia kuweza kunadi itikadi zao na kuwachachamua wapigaji kura wakati wa kampeni za uchaguzi. Kadhalika, wameweza kuunda vikundi vya wasanii ili kuwapigia upatu. Isitoshe, katika nyakati hizi zinazoshuhudia ugumu

wa maisha unaotokana na hali ngumu za kiuchumi ambapo jamii aghalabu hupenda kuburudishwa kwa nyimbo, mashairi au hata mazungumzo yanayoweza kuwatuliza mioyo na kuwasahaulisha, ingawa kwa muda, machungu ya maisha. Ucheshi ni njia moja inayoweza kuleta tiba ya kisaikolojia. Hii ndio maana wasanii kadha siku hizi nchini Kenya wanajitokeza kuwaburudisha watu kwenye kumbi za starehe kwa kutumia vichekesho, mizaha na soga. Mfano mahususi ni kama ule ujulikanao kama "Churchil Live" kwenye runinga ya NTV.

Tunapozingatia utanzu wa ushairi, ukweli ni kwamba sanaa hii imeishia kufunzwa shuleni tu na kusikika kwenye mashindano ya michezo ya kuigiza ama ya kitaifa au miongoni mwa shule mbalimbali. Ni nadra kuona utanzu huu wa fasihi ukitumiwa katika kumbi mbalimbali kuburudisha watu. Hapa tuelewe kwamba mnyambuko mwingi wa maneno tunayotumia katika Kiswahili sanifu yametokana na ushairi. Aidha, misemo na methali kadha tunazotumia leo zilitokana na kauli za kuhekimisha za baadhi ya magwiji wa ushairi wa kale. Je, utanzu wa ushairi unaweza kutumiwa kujenga uwiano na utangamano katika taifa hususan la Kenya? Hili ndilo swala muhimu linalojadiliwa katika makala haya. Swala la utangamano wa kitaifa ni swala zito ambalo hivi sasa linatuturisha, linafikirisha na kushughulisha akili za wengi hata viongozi serikalini. Katika kulijadili swala hili, hatuna budi pia kufuata nyayo za historia yetu ili kuona jinsi utangamano na umoja wa jamii ulivyojengwa, na hasa mchango wa fasihi katika kutambua thamani hizi za kijamii.

### 1.1 Ujenzi wa Utangamano: Mtazamo wa ushairi wa Kiswahili kihistoria

Ujenzi wa utaifa unahusu ujenzi wa utambulisho mmoja kutoka katika utambulisho finyu wa makabila mbalimbali. Unahusu matumizi ya pamoja ya rasilimali za nchi kwa njia ya haki itakayoweza kujenga umoja na utangamano mzuri bila uonevu, ubaguzi, manyanyaso na hila. Je, utangamano ni nini hasa? Huu unaweza kumaanisha watu au jamii mbalimbali kuja pamoja kushirikiana, kuungana na kufanya mambo kwa pamoja kukiwemo pia kuelewana au kupatana. Kulingana na Attafuah (2012:89), utangamano wa kitaifa unahusu uhusiano mzuri wa kijamii uliojengwa juu ya mhimili mkuu wa amani. Utangamano huu wa kitaifa unaweza kujengwa pia kwa kuzingatia usawa katika ugavi wa rasilimali na mali asili kwa jamii zote za nchi bila ubaguzi ili kuhakikisha kupanda kwa thamani ya maisha katika pembe zote za nchi. Kuimarisha amani na utulivu miongoni mwa jamii zenye asili mbalimbali si jambo rahisi. Hata hivyo, ni jambo mustahili kujaribu kujenga amani hiyo chini ya vivuli vya ukabila, ubahili na ufisadi. Utangamano pia huhusisha kukuza na kulinda haki za binadamu kama zinavyofafanuliwa katika katiba ya nchi ili kuhakikisha uwiano mzuri miongoni mwa jamii mbalimbali.

Uzingativu wa uwazi na uwajibikaji ili kutokomeza sera za kiimla na kibinafsi huweza kutuhakikishia utangamano mzuri wa kijamii. Aidha, kuhakikisha usalama wa mtu binafsi popote pale anapoishi na usalama wa umma kwa ujumla ni nguzo muhimu katika kujenga utangamano miongoni mwa watu wa asili mbalimbali. Utangamano mzuri pia ni ule unaotokana na uimarishaji wa uhuru wa kijamii na kisiasa utakaochangia kuwepo kwa jamii tulivu inayojiamini. Hali hii ndiyo inayosababisha kushiriki katika mifanyiko ya uongozi wa nchi katika viwango mbalimbali vya kitaifa. Kwa ujumla basi, masuala muhimu kama vile haki za kibinadamu, uchumi thabiti, haki ya kufanya kazi, haki za kiafya na elimu ni mambo yanayowezesha jamii zetu kuishi pamoja kwa amani na utangamano. Hii ni kwa sababu yale mahitaji muhimu ya kumwezesha kila mtu kuishi yatakuwa yametimizwa. Hali hii basi ndiyo itakayoweza kupalilia ule mhimili mkuu wa taifa ambao ni amani. Mambo haya yote hayawezi kutimizwa bila kuwa na lugha jumuishi itakayotumiwa kuelewesha watu. Aidha, baadhi ya mambo haya huweza kueleweka zaidi yanapotolewa kwa kutumia sanaa mbalimbali zinazotumia malighafi ya lugha.

Utafiti uliofanywa na Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu nchini Kenya (KNCHR, 2008) ulibainisha kwamba vyombo vya habari, hususan vile vilivyotangaza kwa kutumia lugha za kikabila, vilichangia pakubwa kujenga chuki miongoni mwa jamii mbalimbali na kwa hivyo kuzusha uhasama baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2007 nchini Kenya. Kadhalika, vyombo vya kiteknolojia kama vile simu za mkononi vilitumiwa kusambaza lugha yenye mielekeo hasi na hivyo kuchochea uadui miongoni mwa watu na kutibua amani. Mojawapo ya mapendekezo yaliyotolewa na Tume hii ni kwamba ilihitajika kuwe na miradi endelevu ya elimu ya umma itakayohusu haki za binadamu. Elimu ya umma kama hii ingeweza kufanikishwa na taasisi za umma na mashirika ya kibinafsi ili Wakenya waweze kuzingatia masuala ya kibinadamu (KNCHR, 2008:170).

Tunaporejelea utanzu wa ushairi, tunaweza kusema kwamba wataalamu mbalimbali wametoa fasili mbalimbali kuhusu dhana ya ushairi. Sio lengo la makala haya kutoa fasili mbalimbali za ushairi, lakini itasadifu tukisema kwamba huu ni utanzu wa fasihi unaotumia mpangilio wa lugha ya mkato, ya kipicha na yenye mapigo mahsusi katika kutoa maudhui (Senkoro 1982:36). Aidha, ni ukweli usiopingika kwamba umaarufu wa ushairi hautokani tu na vipengele vya lugha kama vile maneno yaliyochujwa na yanayoweza kuteka hisia za msikilizaji au msomaji bali pia yale yanayosemwa. Haya ndiyo aliyobainisha Kezilahabi (1974) alipochangia katika mjadala kuhusu dhana ya ushairi wa Kiswahili na kukaulisha kwamba, ushairi hutegemea kile kinachosemwa na jinsi kinavyosemwa.

Ushairi umekuwa ukitumiwa tangu azali na jamii mbalimbali kuimarisha utamaduni na utangamano miongoni mwa watu. Katika jamii ya Waswahili kwa mfano, tunaweza kupata mifano halisi ya tungo zilizotongolewa ili kuleta hisia za kizalendo. Kihistoria, upwa wa Afrika Mashariki, hususan nchini Kenya, kulikuwa na 'mataifa' madogo madogo au milki za kimji zilizotawaliwa na masultani. Aghalabu masultani hawa waliwatumia washairi kujijengea tawala madhubuti kutisha mahasimu wao au hata kujipigia upatu. Uhasama miongoni mwa milki hizi lilikuwa jambo la kawaida ambapo vita vingi viliendelezwa na viongozi kwa sababu mbalimbali zikiwemo zile za kibiashara. Tungo za washairi hao wa zamani ziliwafanya wenyeji kushabikia uzalendo hasa walipohamasishwa dhidi ya adui. Tungo hizi pia ziliweza kuimarisha uwiano na utangamano wa wanajamii katika milki hizo, ambao walihisi kuwa kitu kimoja na hivyo kuimarisha 'utaifa' wao. Wakati mwingine washairi hao walitumiwa kama vipaza sauti na vikaragosi vya watawala ili kuzua chuki na vita miongoni mwa tawala mbalimbali.

Mifano mahsusi tunaweza kuipata katika milki za kimji zilizokuwa kaskazini mwa upwa wa Kenya, vikiwemo visiwa na maeneo kama vile Mvita, Amu, Pate na Siyu. Ushairi ulitumiwa na manju wa kale kama vile Zahidi bin Mngumi (1758-1828), Muyaka bin Haji (1776-1840), Bakari bin Mwengo (1760-1830), Ali Athman (1776-1834) aliyejulikana pia kama Ali Koti, Muhammad bin Shee Mataka Al-Famau (1825-1868), kwa kutaja wachache. Baadhi ya tungo za washairi hawa wasifika zilichangia kuleta mshikamano wa miliki na 'mataifa' yao.

Muyaka bin Haji, mbali na kwamba alikuwa mshairi msifika, alikuwa pia shujaa wa kivita aliyepigania taifa lake la Mvita. Baadhi ya wahakiki wa mshairi huyu wametoa kauli kwamba hakuwa mzalendo kwani alipowapigania Al-Mazrui waliotawala Mvita, alifanya hivyo kwa sababu za kibinafsi. Alijenga ukuruba mkubwa na magavana wa kimazrui ili kuendeleza biashara yake na alipotunga mashairi kusifia taifa lake la Mvita, basi alifanya hivyo kwa maslahi ya kibinafsi. Hata hivyo, tunapochunguza tungo zake, na hisia zilizosheheni katika tungo hizo, tunaweza kusema kwamba alichangia pakubwa kuhamasisha taifa na watu wake dhidi ya adui kama vile watawala wa Amu. Baadhi ya tungo zake zenye kuashiria uzalendo na utaifa ni kama hizi zilizonukuliwa na Abdulaziz (1979): 'Kongowea ja Mvumo' (uk.19-20), 'Gongwa la Mwana Mkisi' (uk.12), 'Mwina wa Chiza' (uk.143).

Ali Athman (Ali Koti) aliyeishi Pate pia alitumiwa na viongozi kukashifu viongozi wengine. Mfano mahususi ni ule ulionukuliwa na Chiraghdin (1987:31-32) ambapo Ali Koti aliyekuwa pia rafiki mkubwa na Fumo Luti nduguye mfalme wa Pate aliyejulikana kama Ahmed Nabhany, alitunga shairi la kumkashifu mfalme huyo. Chiraghdin anaeleza kwamba, Fumo Luti aligombana na nduguye kisha

akaandamana na Ali Koti kuhamia Siyu kwa Bwana Shee Mataka aliyekuwa mfalme wa Siyu. Uhasama wa Siyu dhidi ya Pate ulishamiri. Vitisho vya kushambuliwa na Siyu viliwaunganisha Wapate ambao walifunga lango la mji na kuruhusu watu kuteka maji tu kisimani nje ya lango. Wapate hawakulima lakini Wasiyu walilima na kuvuna. Hapo ndipo Ali Koti, kupitia maelekezo ya Fumo Luti, alipotunga shairi lililoandamana na mzigo wa mtama kwa watu wa Pate. Mzigo na shairi hilo lililojulikana kama 'shairi la mzigo' viliachwa kisimani. Hivyo, Ali Koti alifaulu kuwachezea shere jamaa zake lakini pia akafaulu kujenga ushikamano wa Wapate dhidi ya adui.

Mbali na tukio hili, Ali Koti aliwahi pia kutumiwa na mfalme wa Pate akatunga 'shairi la mfano' ili kumdhihaki mfalme wa Siyu. Lakini Ali Koti alipokwenda Siyu kuhudhuria karamu, mfalme wa Siyu aliagiza akamatwe ili amwadhibu. Kupitia kipawa chake cha kutunga mashairi kwa ghibu, Ali Koti alipata uhuru alipotunga shairi hili la ubeti mmoja:

*Licha kuwa langishiwe, hata kama laanguka*
*Ukadhihiri ufawe, pasi na kuumunika*
*Ukipowa sikuliwe, kwani halikupunguka*
*Shahasi linganguka, halitwi ina lingine*

Shairi hili la mfano lilikuwa na maana kuwa mfalme hata akatukanwa bado ni mfalme na wala ufalme wake haupunguki.

Historia inatuonyesha pia kwamba katika kisiwa cha Amu kulikuwa na makundi mawili ya kisiasa, Suudi na Zeina, yaliyokuwa yakizozana mara kwa mara. Hata hivyo, iliwabainikia kuwa walihitaji kuungana ili waweze kushinda mahasimu wao ambao kwa wakati huu walikuwa Wa Mvita na Wa Pate. Ushairi ni chombo adhimu walichotumia ili kuleta mshikamano wao. Waliandikiana mashairi mpaka wakapatana na kuwa kitu kimoja (Chiraghdin 1987:11). Mshairi Zahidi Mngumi aliyekuwa pia mtawala wa Amu alitumia kipawa chake kujenga umoja na utangamano wa Wa Amu. Kama anavyoeleza Chiraghdin (1987: 13), mbali na kwamba alitunga mashairi ya kuwatia moyo watu wake ili kuwa na hamasa ya kulinda mji wao, aliheshimiwa pia katika ngoma za Waswahili kama vile gungu na diriji. Ni katika ngoma hizi ambapo tungo za kishairi zilitungwa ili kuimarisha umoja na utangamano wao.

Katika karne iliyopita, washairi wa Kiswahili pia waliendeleza utunzi wa mashairi kama njia moja ya kujenga umoja na utangamano wa kitaifa. Mfano madhubuti tunaoweza kuutoa hapa ni kutoka katika nchi jirani ya Tanzania. Katika harakati za kujenga falsafa ya ujamaa na kujitegemea nchini humo chini ya uongozi wa

aliyekuwa rais wa nchi hiyo Mwalimu Julius Nyerere, ushairi ulitumiwa ili kuvumisha hasa lile Azimio la Arusha la mwaka wa 1967. Mshairi Mathias Mnyampala aliasisi kipera cha ushairi kilichojulikana kama ngonjera ili kutekeleza jukumu hili. Ngonjera ni aina ya mashairi ya kujibizana, mashairi ambayo husheheni malumbano, udahili na utendaji. Awali mashairi haya yalijulikana kama Ngonjera za UKUTA kutokana na chama kilichojulikana kama chama cha Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania. Chama kilichoasisiwa kwenye mwaka wa 1965. Ngonjera zilianzishwa mwaka wa 1964 na hata kabla ya Azimio la Arusha na ziliposhika kani, zilitumiwa kusambaza azimio hili hata baadaye zikaja kujulikana kama ‘ushairi wa kulitangaza Azimio la Arusha na Utamaduni wa Taifa.

Kuna tumbi zima ya mashairi ya karne iliyopita ambayo ilisawiri hali za kijamii, na hivyo kuichachawiza na kuifikirisha jamii ili kujenga ushirikiano na umoja unaohitajika. Tofauti za kitabaka pia zimewahi kusawiriwa kishairi ili kuitanabahisha jamii dhidi ya ubinafsi. Tazama ubeti ufuatao ulionukuliwa na Senkoro (1982:45) kutoka katika *Malenga wa Bara*:

*Nikumbuke (mwanangu) unapostaftahi*
*Penye meza ya msaji*
*Kiti cha godoro*
*Unapoletewa*
*Gudulia la maziwa*
*Paja la kuku*
*Vidani vya nguruwe*
*Mlima wa mayai*
*Kwenye vyombo vya sini…*

Kutokana na mifano hii, ni wazi kwamba nchi yoyote inayothamini maendeleo ya watu wake, haina budi kuwahusisha katika kukumbatia maendeleo hayo. Njia moja ya kuwahusisha katika mifanyiko na michakato ya maendeleo ni kuwajuvya masuala ya kitaifa na yale yanayojiri katika medani za kimataifa. Mojawapo ya njia za kuwajuvya ni kupitia kwa fasihi zetu. Hivyo basi, matumizi ya tanzu za fasihi kama vile ushairi huweza kutumiwa kupitisha ujumbe wa kuimarisha utangamano na amani katika taifa. Kama alivyosema Mwalimu Nyerere (Liundi 2012:68), “Ni kupitia kwa umoja tunapoweza kuwa na uhakika kuwa Afrika inajitawala yenyewe”

(Tafsiri yetu).

Tufahamu pia kwamba matukio ya zamani huweza kuijuvya jamii ya leo na kuumba jamii ya kesho inayoweza kutegemewa. Hivyo, ushairi unaweza kutumiwa kujenga mshikamano na umoja wa kitaifa kupitia kwa nyenzo mbalimbali.

## 2.0 Ushairi wa Kiswahili kwa sasa

Tangu mataifa ya Afrika ya Mashariki kupata uhuru katika miaka ya 1960, suala la utangamano wa kitaifa limeweza kuzishughulisha kalamu za watunzi wa ushairi wa Kiswahili. Tuelewe pia kwamba hivi sasa Kiswahili ni lugha ya jamii moja kama ilivyokuwa katika karne zilizopita. Hii ni kwa sababu lugha hii huzungumzwa na idadi kubwa mno ya watu Afrika ya Mashariki. Sawia na dhima hiyo, ushairi wa Kiswahili umekuwa ukiendeleza na kustawisha matumizi ya lugha hiyo na pia kushughulikia masuala ya kijamii na kitamaduni kama vile utangamano wa kitaifa. Mashairi hayo yamekuwa yakitungwa kwa kuzingatia uhalisi wa maisha ya watu na utamaduni wao.

Kabla na hata baada ya mataifa hayo kupata uhuru, mabadiliko mbalimbali ya kijamii na kitamaduni yameweza kushuhudiwa na kuathiri mkondo wa maisha ya watu. Matokeo yake ni kwamba, watu katika mataifa hayo wameweza kupoteza au kukosa mwelekeo kuhusu maisha yao. Katika karne hii kwa mfano, nchi ya Kenya imeshuhudia vurumai na ghasia za kikabila zinazotishia usalama wa nchi. Katika hali hii, ushairi wa Kiswahili umeweza kuwasilisha kwa ubunifu matatizo yaliyopo na kutoa mwelekeo unaopaswa kuzingatiwa. Suluhu inayotolewa na wasanii hao ni ile yenye chemichemi yake katika utamaduni wao wa asili. Katika utunzi na uwasilishaji, tungo hizo huzingatia mitindo tofauti lakini yenye lengo moja la kubainisha jinsi utangamano wa jamii ya sasa unavyoweza kushughulikiwa. Kwa hivyo, tungo hizo anuwai zimekuwa zikichochea hisia za watu ili kufikia mwafaka unaohitajika.

Katika kubainisha harakati mbalimbali za ujenzi wa utangamano wa jamii, mifano michache ya mashairi ya wasanii kutoka Kenya imezingatiwa huku ikieleweka kuwa kuna utajiri mkubwa wa mashairi yanayotungwa kila uchao ili kufisha hisia za utengano na kuimarisha utangamano wa kitaifa. Mifano ya wasanii hao ni kama vile Abdilatif Abdalla, Alamin Mazrui, Kithaka wa Mberia, Walla bin Walla, miongoni mwa wengine. Baadhi ya mada ambazo zimeshughulikiwa na ambazo zinahusiana na ujenzi wa jamii ya mshikamano ni kama vile: uzindushi wa jamii, umoja katika jamii, masuala ya kisiasa, nafasi ya mwanamke katika jamii, umuhimu wa subira na matumizi ya kauli zinazofaa.

### 2.1 Uzindushi wa Jamii

Kupitia kwa baadha ya mashairi ya Kiswahili ya sasa, jamii imejengewa mandhari ya kujisaili na kujitafakari ili kufikia uamuzi unaofaa kuhusu maisha kwa jumla. Kwa mfano, shairi la 'Jipu', katika *Sauti ya Dhiki,* (Abdalla, 1973:7-8), mshairi anamtaka kila mja asikubali kuchukulia mambo kiholela. Kwa hivyo, juhudi za kujenga furaha katika jamii zinatokana na mtu binafsi. Mtu anapokuwa mwenye furaha ataweza kushiriki vizuri katika harakati mbalimbali za kijamii. Ingawa mtunzi amelichukulia jipu kama tatizo la kibinafsi, anaashiria matatizo ambayo

yapo katika jamii. Kwamba, jamii haiwezi kuwa na utangamano unaofaa iwapo kuna mazonge yaliyosakini. Matatizo hayo sharti yaondolewe bila huruma kama anavyobainisha hapa:

*Jasho jembamba litoke, ndiya mbili likitona*
*Na hapo mtetemeke, si kwa baridi kuona*
*Bali kwa utungu wake, utakaozidi sana*
*Hapa ndipo mtasona, na moyo kufurahiya* (Ubeti wa 10)

Jambo ambalo linabainishwa hapa ni kwamba, jamii isihofu kuchukua hatua ya kutokomeza matatizo pindi yanaposhuhudiwa. Ipo haja ya kuvumilia machungu ilimradi hali nzuri ipatikane. Kwa kufanya hivyo, mazingira ya jamii yatakuwa pahali pema pa kuishi. Mawazo hayo pia tunayakuta katika shairi la 'Bara Jingine' katika *Bara Jingine* (Mberia, 2001:10-16). Katika shairi hili, mtunzi ameonyesha kuwa taifa lake, halikutarajia kuuondoa ukoloni na kuurejesha utawala huo huo kwa sura nyingine ya ukoloni mamboleo. Kulingana na mtunzi, ndoto yao ilikuwa 'tamu kama asali' lakini ndoto hiyo ilijengewa mizengwe na 'genge la nzige'. Kadhalika, 'usalama wa taifa' ulikuwa wa 'kulinda mamba wa ikulu'. Taswira inayowasilishwa si ile iliyowahamasisha wanajamii kupigania uhuru wao.

Kutokana na hilo, mtunzi anatoa shime kwa jamii kutoizika ndoto yao hadi pale taifa litakapokuwa pahali pema pa kuishi. Kama wazalendo, raia wa nchi hawahitaji kuukimbia uhalisi huo bali matatizo yaliyopo yanahitaji kutafutiwa dawa mjarabu hadi ndoto yao itakapotimizika. Kwa sababu hiyo, wananchi wanahimizwa kuchangia katika kuleta suluhu la sivyo, nchi yao itakuwa jehanamu. Hata hivyo, safari hiyo huwa ni ngumu na ya lazima kama inavyobainishwa katika shairi la 'Wasafiri Tuamkeni' katika *Sauti ya Dhiki* (Abdalla 1973:67-68). Hapa jamii inafahamishwa kuwa safari hiyo ni ya lazima kwa kila mja:

*Ni ndiya yenye msitu, na mirefu miti yake*
*Imefaa nyama mwitu, kila mmoja na pake*
*Na walionapo kitu, ni lazima wakishike*
*Huu ndiwo mwanzo wake, siwo mwisho wa safari* (Ubeti wa 4)

*Japo ni ngumu safari, wendaji tusigutuke*
*Ingawa ina hatari, twendani tusitishike*
*Ingawa ndefu safari, lazima imalizike*
*Huu ndiwo mwanzo wake, siwo mwisho wa safari* (Ubeti wa 6)

Naye Mazrui (1988:30) katika shairi la 'Kilio cha Afrika' lililoko katika *Chembe cha Moyo* anazisihi jamii za Afrika kulienzi bara au taifa kwa heshima na taadhima inayostahili. Tusipofanya hivyo, tutachekwa na mabara mengine.

**2.3 Umoja katika Jamii**

Suala la umoja wa taifa limekuwa likishughulikiwa siyo tu katika vyombo vya habari bali pia limekuwa likihimizwa katika ushairi wa Kiswahili. Kama tulivyogusia awali, swala la ukabila limekuwa kikwazo kikubwa katika shughuli za maendeleo ya taifa. Kwa mfano, pale kabila moja linapojiona bora zaidi likilinganishwa na jingine, hali hii husababisha hisia za udunishwaji hasa kwa yale makabila madogo. Kadhalika, mtu binafsi huweza kujenga mwelekeo wa kibinafsi ambapo masuala ya kijamii huweza kutatizika. Mashairi ya Kiswahili yamekuwa yakibainisha upotovu huo huku yakiwataka watu kushirikiana katika shughuli zao. Kwa mfano, shairi la 'Mnazi Vuta N'kuvute' katika *Sauti ya Dhiki* (Abdalla, 1973:17-22) linahimiza umoja miongoni mwa wanajamii. Kulingana na mtunzi , watu wanahitaji kushirikiana ili jamii iweze kujengwa katika misingi ya umoja, upendo na utangamano. Suala hili linasawiriwa kupitia kwa ubeti ufuatao:

*ALII*
*Mnazi ni wa shirika, mimi na wewe mwendani*
*Ushakuwa wataka, kunitowa shirikani?*
*Hilo halitatendeka, wala haliwezekani*
*Sikutaali abadani* (Ubeti wa 7)

Katika muktadha wa ubeti huo (na shairi zima kwa ujumla), mshairi ameidhihirishia hadhira kwamba iwapo baadhi ya watu katika jamii watasukumwa na tamaa, basi watachukuliwa kuwa maadui wa umma. Ubinafsi huo unakuwa kama donda ndugu ambalo linahatarisha utangamano wa jamii. Katika muktadha huo pia, mhusika Alii anamchukulia mwenziwe (Badi) kuwa mja asiyepigwa mshipa na dhiki zinazomwandama. Hapo mwanzoni kabla ya kufariki kwa wavyele wao, Alii na Badi waliishi kwa undugu lakini kutokana na tamaa ya mali na uongozi, hali hiyo ilizua kiburi na kutojali. Badi anakuwa na ubinafsi uliokithiri. Suluhu inayotolewa ni kuwa, watu wanahitaji kuelekezwa ili kujenga maridhiano na uwezo wa mtu usiwe ni kikwazo. Hili ni tatizo ambalo hulikumba tabaka lenye uwezo wa kiuchumi ambapo halijui wala kutambua dhiki zinazoliandama tabaka la chini.

Suala hili pia limeshughulikiwa katika shairi la 'Mrako wa Nyuki' katika *Bara Jingine* (Mberia, 2001:20-25). Katika shairi hilo, ujumbe umewasilishwa kimaelezo na kwa taswira ya kimaono. Kwamba, umoja ni nguvu ilhali utengano ni udhaifu. Jamii inayosawiriwa ilikuwa ikiishi kwa umoja huku utamaduni wake ukiielekeza. Maadui au wageni walipowavamia na kutamakani katika mastakimu yao, wenyeji ambao hapa ni 'nyuki' walifadhaishwa mno na vitimbi vyao. Swali ni kwamba, wangewaondoa vipi adui hao? Baadhi yao walishirikiana nao, wengine wakaamua kupambana nao. Juhudi hizo hazikufua dafu. Mwafaka wa kuwaondoa maadui hao ulipatikana wakati jamii ilipotambua umuhimu wa umoja. Mtunzi anatuonyesha kwamba, suala la ushirika wa jamii limekuwa likihimizwa mno katika utamaduni wao.

Katika beti za shairi hilo, wadudu kama vile 'nyuki' wametumiwa ili kubainisha zaidi ujumbe wa msanii. Jambo linalosailiwa ni kwamba iwapo wadudu hao wameweza kutenda maajabu kutokana na utambuzi wa ushirika, kwa nini wanadamu wasiweze kuiga mfano huo? Kadhalika, shairi la 'Muosheni' katika *Sauti ya Dhiki* (Abdalla, 1973:75-76) linapiga mwangwi wa ujumbe uo huo:

*Simwateni, ati sababu afile*
*Ni kanuni, ya tangu zama za kale*
*Muosheni, mabuu yande yamle* (Ubeti wa 4)

Ubeti huo unashadidia wazo kwamba, katika jamii kuna baadhi ya watu ambao bado hawajautambua umuhimu wa ushirika. Watu kama hao hawapaswi kuachwa bali wanahitaji kutanabahishwa ili wao pia waweze kuacha ubinafsi wao. Aidha, ujumbe unaohusu kuhamasishana katika jamii unatiliwa nguvu katika shairi la 'Nieleze' katika *Bara Jingine* (Mberia, 2001:53-54). Mshairi anasema ni muhimu kuzungumza na wenzetu kwa uzuri ili kuweza kutambua manufaa ya umoja katika jamii.

### 2.4 Masuala ya Kisiasa

Kulingana na katiba za nchi, watawala na watawaliwa wana haki sawa kuhusu masuala ya utawala. Hata hivyo, baadhi ya watu wanapoteuliwa kushika hatamu za uongozi, hujiona kuwa ni 'miungu wadogo' katika taifa. Kadhalika, wanapopata madaraka hayo, hujichukulia kuwa bora zaidi kuliko wengine. Kutokana na kiburi hicho, hawataki kuonywa wala kuelekezwa. Baadhi ya watunzi wa ushairi wa Kiswahili huwaona wale wenye mielekeo hiyo kuwa visiki vya utangamano wa jamii. Suala la uongozi pia linahitaji mtu ambaye amejitolea kama mzalendo halisi. Shairi la 'Mamba' *Sauti ya Dhiki* (Abdalla, 1973:10) limesawiri mambo yanayohusu uongozi dhalimu katika jamii. Utawala huo aghalabu huzua hofu na kusababisha uvurujuaji wa haki za kimsingi. Utangamano basi, unakuwa ndoto tu isiyo na uhalisi wowote. Mshairi anasawiri hali hii miongoni mwa watawala:

*Kuna mamba, mtoni metakabari*
*Ajigamba, na kujiona hodari*
*Yuwaamba, kwamba 'taishi dahari'* (Ubeti wa 2)

*Memughuri, ghurari za kipumbavu*
*Afikiri, hataishiwa na nguvu*
*Takaburi, hakika ni maagavu* (Ubeti wa 3)

Kupitia kwa beti hizo, ni dhahiri kwamba kiburi cha baadhi ya viongozi huweza kusambaratisha jamii. Kiongozi anapopata wadhifa huo, hujiona ni tofauti kabisa na watawaliwa. Hawezi kujenga mlahaka mzuri na watawaliwa. Watu humwogopa, hawana uhuru wa kutoa mawazo yao kwa kuhofia usalama wao.

Uelekezi unaotolewa katika shairi hilo ni kwamba watawala na watawaliwa wanapaswa kuelekezana katika harakati za maendeleo ya jamii. Aidha, shairi la 'Unafiki' katika *Malenga wa Ziwa Kuu,* (Walla, 1994:46) linasawiri hali hii ambayo huweza kufisha utangamano wa kijamii.

## 2.5 Nafasi ya Mwanamke katika Jamii

Katika jamii ya leo na kulingana na katiba ya nchi, mwanamke na mwanamume wana nafasi sawa katika harakati mbalimbali za kijamii. Hali hii na juhudi za wanawake katika kuufikia usawa wa kijinsia. Tafiti mbalimbali za usawiri wa wanawake katika matini za fasihi ya Kiswahili zimefanywa na wasomi mbalimbali katika janibu za Afrika Mashariki kama vile Momanyi (1998), Wandera (1996), Mule P.K. (1991), Muindi (1990), Sirucha (1986), miongoni mwa wengine. Baadhi ya tafiti hizi zimebaini kwamba katika tamaduni nyingi za kiasili barani Afrika, mwanamke hakutarajiwa kushika hatamu za uongozi wala kushiriki katika shughuli za kiuchumi. Tofauti za majukumu kati ya wanaume na wanawake yalibainishwa wazi na jamii husika, hususan jamii za kuumeni. Ieleweke pia kwamba, mitafaruku na mizozano baina ya wanawake na wanaume huweza kutibua amani katika jamii. Unyanyaswaji wa wanawake umeendelea kuwafanya wengi kukosa nguvu ya kuyadhibiti maswala yanayohusu maisha yao. Hata hivyo, mielekeo hasi kuhusu nafsi ya kike inaendelea kupitwa na wakati. Baadhi ya mashairi yameweza kusawiri hali tofauti kabisa na zile tungo za awali zilizokuwa zikimsawiri mwanamke kama chombo na kifaa tu cha wanaume.

Tukichunguza baadhi ya tungo hizi tunaweza kuona mabadiliko katika usawiri huo. Kwa mfano, shairi la 'Kutendana', katika *Sauti ya Dhiki,* (Abdalla, 1973:89-110), limedhihirisha dhuluma anazofanyiwa mwanamke na hatua anayoichukua. Hapo awali alikubali kuanzisha mahusiano ya kimahaba na mwanamume huku akidhani kuwa mwenziwe anamstahi. Alipobaini mbwembwe na ujanja uliokuwa unaendelea, anaamua kuibana 'dawa' aliyo nayo. Ujanja na vitimbi vya mwanamume dhidi ya mwanamke vimeelezwa pia katika shairi la 'Nakumbuka ulivyokuwa' katika *Bara Jingine* (Mberia, 2001: 76:78). Katika shairi hili, mhusika mwanamke anajikuta katika mtego wa nishai za mwanamume bila kujua. Hata hivyo, mshairi anawalaumu wote wawili kutokana na misukumo yao ya kibinafsi. Mwanamke alikuwa mwenye uchu wa kuingia katika kifungo cha ndoa na mtu mwenye uwezo wa kifedha. Mwanamke huyu alifikiri kuwa ameukata. Muda si mrefu anagundua kuwa, ameambukizwa maradhi ya zinaa. Mtunzi anatoa onyo kwa mwanamume kuwa si vyema kutumia uwezo wa kifedha kama chombo cha kuwaghilibu wenzao wasiojiweza katika jamii. Hali hii huchangia katika kutoelewana miongoni mwa wanajamii. Aidha, jambo hili halijengi muamana mzuri wa kimahusiano bali hutibua amani katika jamii. Iwapo wanawake

watatengwa na kubaguliwa, utangamano wa kijamii hautaimarika kwani wao pia wana mchango mkubwa wa kuleta umoja na amani ya jamii.

**2.6 Umuhimu wa subira katika Jamii**

Baadhi ya watu wamekuwa wakielekezwa kwa pupa katika kufanikisha maisha yao. Hili halipaswi kuwepo katika jamii. Uzingativu wa pupa katika maisha huweza kumfanya mtu au watu kujiingiza katika mambo ambayo si ya kiutu. Mambo ambayo yamekuwa yakishuhudiwa katika jamii ya sasa ni kama ujambazi na wizi wa kimabavu. Vitendo hivyo humshushia mtu hadhi na pia kuudhiki moyo bila sababu ya msingi. Subira hujenga utu wa mtu katika jamii. Kadhalika, mafanikio katika maisha ya mtu hayavutwi kwa kamba. Baadhi ya tungo za kishairi zimekemea hali hii. Kwa mfano, shairi la ‘Zindukani’ katika *Sauti ya Dhiki* (Abdalla, 1973:69-72) linashutumu uendekeza wa subira kiholela. Baadhi ya watu katika jamii anayozungumzia mtunzi wamekuwa wakilaza damu huku wakisubiri Mwenyezi Mungu kuwashushia miujiza na neema. Kulingana na mawazo ya mtunzi, mwelekeo huo haufai kuwaelekeza wanajamii. Katika muktadha huu, mtunzi anamwondolea Mwenyezi Mungu kidole cha lawama. Nasaha ya mshairi huyu ni kwamba, watu wanapaswa kubadili mielekeo yao na kujitahidi jinsi wawezavyo kuboresha hali zao za kiuchumi na katu wasitegemee miujiza wala majaaliwa.

Matokeo ya kuzingatia majaaliwa ni kujifukarisha na pia kuufukarisha uchumi katika kiwango cha mtu binafsi na jamii kwa ujumla. Shime inayotolewa ni kutosita juhudi za kujishusisha zaidi katika harakati za kuimarisha maisha yao la sivyo, michirizi hiyo ya dhiki itadumaza ndoto ya maendeleo katika jamii. Mfano unaotolewa ni ule wa ‘upanzi wakati wa mvua’ ili wakati wa kiangazi watu wapate ‘kitu cha kuwafaa’. Kwa hivyo, juhudi za kila mja ni muhimu katika kulibingirisha gurudumu la maendeleo ya jamii. Subira inayozingatiwa katika shairi hilo ni matokeo ya juhudi ambazo zilifanywa hapo mwanzoni, vinginevyo sivyo.

Kadhalika, mtu anapozingatia subira, hujijengea ngome katika kauli anazozitoa huku akijijengea mikakati ya malengo yake maishani. Suala hili pia limedhihirishwa katika shairi la ‘Mnazi Vuta N’Kuvute’ katika *Sauti ya Dhiki* (Abdalla, 1973:17-22) ambapo mhusika Alii amekuwa akimnasihi Badi kutozingatia ubinafsi ambao huendelezwa na tamaa. Ingawa Alii anapata dhiki katika maisha kutokana na mahusiano yake na Badi, hataki kuelekezwa kwa pupa wala hasira. Hii inatokana na utu na subira aliyo nayo kwa wenziwe katika jamii. Manufaa ya subira katika maisha ya watu yamefafanuliwa pia katika mashairi kama vile‘Subira Huvuta Kheri’ katika *Malenga wa Mvita* (Nassir, 1971:115), na ‘Hasira Hasara’ katika *Chembe cha Moyo* (Mazrui, 1988:23).

**2.7 Matumizi ya kauli zinazofaa**

Kauli zinazotolewa katika mawasiliano ya watu huweza kujenga au kuubomoa utangamano wa kijamii katika taifa. Kwa hivyo, kila mja anahitaji kuwa makini katika matumizi ya ulimi. Shairi la 'Ulimi' katika *Malenga wa Ziwa Kuu,* (Wallah, 1988:37) linasisitiza matumizi mwafaka ya ulimi:

*Katika uneni wako, nena nyuma ya kuwaza*
*Usijezua chafuko, umati ukakubeza*
*Ulimi hasidi yako, hasa unapoteleza*
*Tumia ni chombo chako, kwa akili na kuwaza* (Ubeti wa 3)

Katika ubeti huo kuna mambo muhimu yanayowasilishwa. Baadhi ya mambo hayo ni kama vile kuwaza kabla ya kunena, ulimi huweza kumponza mtu au pia kauli mbaya huweza kusababisha fujo katika jamii. Ujumbe unaowasilishwa basi ni pamoja na mazingatio ya kauli zifaazo ili kuwepo na amani na upendo katika jamii. Kadhalika, heshima ya mtu katika jamii huwa ya kiwango cha chini iwapo ulimi utatumiwa vibaya. Mtu anaporopoka maneno bila ya kuzingatia hekima, watu humbeza na haaminiki katika jamii. Shairi la 'Mja si mwema' katika *Sauti ya Dhiki* (Abdalla, 1973:34) limesawiri namna ulimi au kauli zisizofaa zinavyoweza kukosanisha watu. Katika kubainisha madhara ya kauli mbaya, msanii anasema:

*Mja hana haya haya hazimo mwake usoni*
*Mja ni mbaya hutimba shimo ungiye ndani*
*Na ukisha ngiya azome zomo furaha gani!*
*Mmoja kwa miya ndiye hayumo baya kundini*
(Ubeti wa 6)

Pamoja na kutumia kauli zinazofaa, kuna haja ya kusema kweli badala ya uongo. Watu wanaposema kweli husaidia kujenga upendo na imani katika jamii.

**3.0 Hitimisho**

Makala haya yamefafanua jinsi ushairi wa Kiswahili unavyoshughulikia suala la utangamano na ujenzi wa kitaifa. Mifano michache ya mashairi imezingatiwa ili kushadidia zaidi hoja zilizotolewa. Kutokana na hoja zilizotolewa, ni dhahiri kwamba ushairi kama utanzu wa fasihi unaweza kutumiwa kujenga utangamano wa kitaifa. Hivyo basi, hoja inatolewa hapa kwamba ushairi wa Kiswahili ufundishwe katika ngazi zote za elimu ili wanafunzi waweze kuufurahia na kujifunza vito vya hekima vinavyotolewa na tungo hizo. Lingekuwa pia jambo bora iwapo kungekuwa na mashindano ya utunzi, ukariri na uigizaji wa mashairi ya Kiswahili katika shule na vyuo ili mada kama vile utangamano na ujenzi wa taifa ziweze kushughulikiwa ipasavyo katika jamii. Sanaa hii inaweza kujumuishwa katika tamasha na mashindano ya uigizaji na uimbaji katika shule na vyuo. Kadhalika, vyombo vya habari vinaweza kutenga muda zaidi hasa katika vipindi vya Kiswahili ili maswala ya fasihi hususan ushairi, yaweze kupata nafasi

adimu ya kujadiliwa na kuelezwa jinsi yanavyoweza kujenga utangamano wa jamii.

## Marejeleo

Abdalla, A. (1973): *Sauti ya Dhiki*. Nairobi: Oxford University Press.

Abdulaziz, M.H. (1979): *Muyaka: 19th Century Swahili Popular Poetry*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Attafuah, K.A. (2010): "Ethnic Diversity, Democratization and Nation – building in Ghana" katika *Ethnic Diversity in Eastern Africa: Opportunities and Challenges*.K. Njogu, K. Ngeta na Wanjau (Wahariri). Nairobi: Twaweza Communications.

Chiraghdin, S. (1987): *Malenga wa Karne Moja*. Nairobi: Longman Kenya.

Kezilahabi, E. (1974): *Kichomi*. Nairobi: Heinemann Educational Books Ltd.

KNCHR (2008): *On the Brink of the Precipice: A Human Rights Account of Kenya's Post-2007 Election Violence*. Nairobi: KNCHR Report.

Liundi, C. (2012): *Julius K. Nyerere*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers Ltd.

Mazrui, A. (1988): *Chembe cha Moyo*. Nairobi: East African Educational Publishers

Mberia, K. (2001): *Bara Jingine*. Nairobi: Marimba Publications Ltd.

Momanyi, C. (1998): "Usawiri wa Mwanamke Muislamu katika Jamii ya Waswahili kama Inavyobainika katika Ushairi wa Kiswahili." Tasnifu ya Ph.D. Chuo Kikuu cha Kenyatta. Nairobi. (Haijachapishwa).

Muindi, A. (1990): "Usawiri wa Wahusika Makahaba katika Vitabu vya Said Ahmed Mohamed" Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. Nairobi. (Haijachapishwa).

Mule, P.K. (1991): "Swala la Mwanamke katika Tamthilia ya Mwanamke" Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. Nairobi. (Haijachapishwa).

Nassir, A. (1971): *Malenga wa Mvita*. Nairobi: Oxford University Press.

Senkoro, F.M. (1982): *Fasihi*. Dar es salaam: Press and Publicity Centre.

Sirucha, B.A. (1986): "Hadhi na Hali ya Mwanamke katika Riwaya za S.A. Mohamed." Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. Nairobi.(Haijachapishwa).

Wandera, S.P. (1996): "Usawiri wa Mwanamke katika Ushairi wa Kiswahili 1800-1900: Uhalisi au Ugandamizwaji?" Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Egerton. Njoro. (Haijachapishwa).